**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA FEDHA**
**WAKALA WA HUDUMA YA UNUNUZI SERIKALINI**

# TAARIFA KWA UMMA

## MABORESHO YA MFUMO WA GIMIS

**Dar es Salaam, 17 Juni, 2025**

Wakala wa huduma ya Ununuzi Serikalini (GPSA) unapenda kuwataarifu kwamba kutakuwa na zoezi la kuboresha mfumo wa **GIMIS tarehe 20 Jun**i, **2025** kuanzia saa tano kamili (5:00) usiku hadi saa kumi kamili (10:00) alfajiri. Katika muda huo, huduma kupitia mfumo wa GIMIS hazitapatikana.

Maboresho haya yanalenga kuboresha utendaji kazi wa mfumo wa GIMIS pamoja na kuwezesha kubadilishana kwa taarifa (Integration) kati ya mfumo wa NeST na GIMIS ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za Wakala kupitia mfumo wa NeST.

Kukamilika kwa maboresho haya ya mfumo kutawezesha matumizi ya namba ya malipo (*Control Number*) moja kwa kila 'wallet' kwa ajili ya kuweka bakaa *(Deposits)* kwa huduma ya mafuta na vifaa. Pia maboresho haya yatawezesha upatikanaji wa 'token' kupitia ujumbe mfupi wa simu (SMS), hivyo mnaombwa kuwasajili au kuboresha taarifa za watumishi wa kada ya udereva kwenye mfumo wa GIMIS ili kufanikisha mtumishi husika kupokea 'token' ya mafuta au vifaa kupitia ujumbe mfupi wa simu.

Aidha, ili kufanikisha upatikanaji wa huduma za Wakala katika mfumo wa NeST, Taasisi Nunuzi kupitia Idara Tumizi (*User Department*) zitapaswa kuboresha taarifa zake za 'Cost Centre' au kutengeneza 'wallet' mpya katika mfumo wa NeST.

Kwa msaada zaidi tafadhali wasiliana nasi kupitia barua pepe ya "**support@gpsa.go.tz**" au kupitia kituo chetu cha huduma kwa mteja kwa njia ya simu namba **+255 735 005 005**.

Wakala unaomba radhi kwa usumbufu wowote utakaojitokeza.

Imetolewa na
**KITENGO CHA MAWASILIANO NA MASOKO**